## 1. UTANGULIZI

Matumizi ya Huduma ni mwongozo wa matumizi na utoaji wa huduma kupitia mfumo wa kuendesha skuli, SchoolMtandao. Lengo ni kuhakikisha uwazi, uwajibikaji, na ubora katika utoaji wa huduma za kuendesha skuli kupitia teknolojia. Mfumo huu unasaidia shughuli za kila siku za shule ikiwa ni pamoja na usimamizi wa wanafunzi, madarasa na malipo.

## 2. MAONO

Kuwa mfumo bora wa kuendesha skuli kwa njia ya kidijitali, unaowezesha skuli kutoa huduma bora za elimu kwa ufanisi na uwazi.

## 3. DHAMIRA

Kutoa huduma za kiteknolojia za kuendesha skuli ambazo ni salama, rahisi kutumia, na zinazoboresha utoaji wa elimu kwa kushirikisha wadau wote kwa njia ya uwazi na ufanisi.

## 4. WATEJA WETU NI NANI?

- Wamiliki wa Skuli
- Wahasibu
- Wazazi/Malezi

## 5. HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MFUMO

- Usajili wa wanafunzi
- Usimamizi wa madarasa
- Malipo ya ada na taarifa za kifedha
- Ripoti wanafunzi na malipo
- Maktaba ya kidijitali na nyaraka muhimu

## 6. HAKI ZA WATUMIAJI

Watumiaji wa mfumo huu wana haki ya:

- Kupata huduma kwa wakati na kwa usahihi
- Kupata taarifa zao binafsi kwa uwazi
- Kulindwa kwa usiri wa taarifa zao
- Kupata msaada wa kiufundi kwa wakati

Swahili Technologies

- Kutoa maoni au malalamiko kuhusu huduma

## 7. WAJIBU WA WATUMIAJI

Watumiaji wa mfumo wanawajibika:

- Kutumia mfumo kwa njia sahihi na kwa madhumuni yaliyokusudiwa
- Kulinda jina la mtumiaji na nywila (password)
- Kuripoti matatizo ya kiufundi kwa wakati
- Kutii sheria na kanuni za shule zinazohusiana na matumizi ya teknolojia
- Kuhifadhi taarifa kwa uadilifu na kuepuka usambazaji wa taarifa za uongo

## 8. NJIA ZA KUTOA MAONI AU MALALAMIKO

Watumiaji wanaweza kutoa maoni au malalamiko kupitia:

- Barua pepe: info@schoolmtandao.co.tz
- Simu: +255 777 118462

## 10. UBORESHAJI ENDELEVU

Tunaahidi kuboresha mfumo wetu kwa kuzingatia maoni ya watumiaji, mabadiliko ya teknolojia, na mahitaji ya sekta ya elimu.

---

## 11. HITIMISHO

Tunathamini ushirikiano wa watumiaji wote katika kuhakikisha mfumo huu unatumika ipasavyo na unatoa huduma bora kwa maendeleo ya elimu nchini. Karibu tutumie teknolojia kuimarisha elimu!

Swahili Technologies